# KUJIANDAA KUANZA SHULE

**Kuanza shule huleta mabadiliko makubwa kwa watoto na familia. Kuzoea watu wapya, maeneo na taratibu kunaweza kusisimua – na vile vile kuleta changamoto. Kuna mengi unayoweza kufanya ili kumsaidia mtoto wako aanze shule vizuri.**

## Mwanzo mzuri wa shule ni nini?

Familia na walezi ndio waalimu wa kwanza wa watoto. Mambo unayofanya nyumbani pamoja na mtoto wako humsaidia kujifunza na kukua na humtayarisha kwa shule. Njia bora ya kumsaidia mtoto wako kujifunza na kukua ni kupitia **kucheza**.

Mwanzo mzuri wa shule husaidia watoto wajifunze vizuri na wafurahie zaidi. Na watoto wanapofurahia kuwa shuleni, wanapata shauku ya kutaka kuendelea kusoma. Shule ya mtoto wako itajitahidi ili kukidhi mahitaji ya kibinafsi ya mtoto wako, na kutumia usaidizi wa ziada ikiwa unahitajika. Unaweza pia kumsaidia mtoto wako kwa kufanya mambo yanayomsaidia kuzoea shule na ahisi salama, kujiamini na kushikamana.

## Chezeni na mjifunze nyumbani

Kucheza ndiyo njia bora ya kumsaidia mtoto wako kujifunza. Kucheza hukuza ujuzi wa kudumu katika hisabati, kama vile kuhesabu, kupanga, kuweka katika makundi na kupanga kwa ukubwa. Kucheza humsaidia mtoto wako kugundua asili na sayansi na kumwezesha awe mbunifu. Mtoto wako anapocheza, anajifunza pia kuhusu hisia na anaboresha ujuzi wake wa lugha na kusoma na kuandika: Hapa kuna baadhi ya mambo mnayoweza kufanya nyumbani:

- **Shughuli za kawaida:** Watoto hujifunza kupitia shughuli za kila siku kama vile upishi, kupanga na kusafisha meza, kutenganisha nguo za kufua, kuondoa nguo na vifaa vya kuchezea, na kutunza mimea na wanyama vipenzi. Unaweza kumsaidia mtoto wako kujifunza kwa kumwuliza maswali, kama vile *'Tunahitaji vikombe vingapi vya unga?'* au *'Unaweza kupata soksi zinazofanana?'*
- **Michezo:** Kucheza michezo rahisi kama vile UNO, Snap, Memory, I Spy, na Kujificha na Kutafutana humsaidia mtoto wako ajifunze na humfundisha kuhusu kuchukua zamu.
- **Vipande vya ujenzi:** Kujenga kwa kutumia vipande kama vile LEGO, vipande vya mbao au masanduku ya kadibodi hukuza ujuzi wa kutumia viungo vidogo vya mwili na humwezesha mtoto wako awe mbunifu na atatue matatizo.
- **Sanaa na ufundi:** Shughuli za sanaa na ufundi pia hukuza ubunifu na huimarisha ujuzi wa viungo vidogo vya mwili na utatuzi wa matatizo.
- **Kuvaa mavazi**: Kuvaa mavazi kuukuu na kujifanya kuwa wahusika tofauti hujenga ubunifu na ujuzi wa lugha.
- **Muziki, hadithi na densi:** Kusoma, kusimulia hadithi, kusikiliza na kucheza muziki, na 'kutafuta hazina' ili kutafuta vifaa karibu na nyumba au bustani yote hujenga ujuzi wa lugha ya mtoto wako.
- **Michezo ya nje:** Kutembea, kupanda vilima, kuendesha baiskeli au skuta, kwenda kwenye uwanja wa michezo, kujenga vyumba vidogo, kurusha na kudaka mpira, kupiga mipira laini

kwa raketi ya tenisi au gongo la kriketi ya mpira laini, kuchimba udongo na matope – yote haya humsaidia mtoto wako kujifunza na kukua.

- **Chunguza na uulize maswali:** Mtoto wako anapocheza, uliza maswali kama vile *'Unaweza kunieleza…?', 'Nashangaa nini kingetokea kama…?', 'Ungejibu swali hilo aje...?'*
- **Ratiba:** Kufanya mambo kwa wakati mmoja kila siku humwezesha mtoto wako kujua mambo ya kutarajia na kumsaidia adhibiti hisia zake. Taratibu humsaidia watoto akabiliane na changamoto za shule. Ni muhimu sana kuwa na utaratibu wa kulala, kwa mfano: kula chajio na kuoga, kuvaa pajama, kupiga mswaki, kusoma vitabu na kisha kwenda kulala.

## Fahamu mambo yanaofanyika shuleni

Kuwa 'tayari kwa shule' hakuhusu kujifunza masomo, bali ni kufahamu mambo yatakayofanyika shuleni na kuwa na matarajio chanya. Hapa kuna baadhi ya mambo unayoweza kufanya ili kumsaidia mtoto wako:

- Shiriki katika mabadiliko yoyote kwenye mipango inayotolewa na chekechea au shule ya mtoto wako.
- Safiri kwenda na kurudi shuleni mara kwa mara.
- Mruhusu mtoto wako acheze na watoto wengine watakaosoma shule moja.
- Himiza kujitegemea kwa kumfundisha mtoto wako jinsi ya kuvaa, kutumia msala, kunawa mikono, kujipaka mafuta ya kujikinga na miale ya jua, na kupanga na kubeba mkoba wa shule.
- Zungumza kuhusu kuanza shule. Mchangamshe mtoto wako kuhusu shule na mzungumzie wasiwasi wake wowote.
- Msomee vitabu au umsimulie hadithi kuhusu kuanza shule.
- Zungumzeni na mfanye mazoezi ya mambo yatakayofanyika baada ya shule.
- Jitayarishe kumchukua na kumpeleka kwa kuangalia saa za kuanza na kumaliza shule na kujua mahali pa kumpeleka na kumchukua mtoto wako.
- Anza kutumia jina la mwalimu, ikiwa unaweza.

## Jinsi chekechea ya mtoto wako itasaidia

Chekechea pia husaidia watoto kujiandaa kuanza shule. Katika chekechea, watoto huendeleza ujuzi kupitia kucheza, kushirikiana na wengine na kupata marafiki.

Mwalimu wa chekechea wa mtoto wako atamsaidia mtoto wako kumaliza chekechea na kuingia shule ya msingi kwa kuandika **Taarifa ya Mpito ya Masomo na Maendeleo (Taarifa ya Mpito).** Taarifa ya Mpito inatolewa kwa shule atakayojiunga mtoto wako. Inafafanua uwezo, nguvu na mambo anayopenda mtoto wako na jinsi anavyojifunza vyema zaidi. Utaombwa kusaidia kujaza Taarifa ya Mpito ya mtoto wako, na mtoto wako pia anaweza kushiriki mawazo na hisia zake.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Taarifa ya Mpito, tafadhali tembelea tovuti ya Idara (tazama hapa chini).

## Pata maelezo zaidi

- Vidokezo vya kuanza shule (education.vic.gov.au)
- Kumaliza chekechea na kujiunga na shule (education.vic.gov.au)
- Jinsi ya kuchagua shule na kujiandikisha (education.vic.gov.au)
- Kuanza shule: kuandaa mtoto wako | Raising Children Network
- Kuanzia Shuleni kwa Afya - Better Health Channel
- Mpito kwa rasilimali za shule kwa familia (education.vic.gov.au)